

HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA



TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI YA UPANGAJI WA BUSTANI YA MWALIMU NYERERE MEMORIAL PEACE PARK

ZABUNI NAMBA LGA/003/2018-2019/NC/10

1. Halmashauri ya Jiji la Arusha inakusudia kupata mpangaji atakaefanya biashara halali katika eneo la bustani ya Mwalimu Nyerere Memorial 'Peace Park'
2. Halmashauri ya Jiji la Arusha inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kuboresha, kulitunza na kufanya biashara katika eneo hilo ili Halmashauri iweze kupata mapato.
3. Mpangaji wa Eneo la bustani ya Mwalimu Nyerere Memorial Peace Park atakaefanikiwa zabuni hataruhusiwa kumpangishia mtu mwingine (Sublets) bali kufanya Biashara yeye menyewe.
4. Zabuni zinashughulikiwa kwa utaratibu wa ushindanishi wa waombaji wenyeji (Preferences to Local Community) kama ilivyoainishwa Kwenye Kanuni za Manunuzi (PPA 2011) – Kanuni ya 40 .GN 446 ya 2013 Kwa hiyo iko wazi kwa waombaji wenyeji wote wa jiji la Arusha.
5. Waombaji wote wenye nia na uwezo wanaweza kupata taarifa kamili kupitia makabrasha ya zabuni katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni ya **Halmashauri ya Jiji la Arusha, barabara ya Boma S.L.P. 3013, Arusha**, kila siku kuanzia saa **2.30 asubuhi hadi saa 9:30 mchana**, siku za Jumatatu hadi Ijumaa [kuondoa siku za sikukuu zinazotambulika kitaifa]
6. Nyaraka za aina zote za Zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada ya Maombi ya Tshs **50,000. (Hamsini Eflu)** Malipo ya maombi ya zabuni kufanyika kupitia akaunti ya Halmashauri ya Jiji la Arusha iliyoko katika Benki ya NMB, tawi la Clock Tower, akaunti ya Jumla Halmashauri ya **jiji Arusha. Account Na 40801200336** na kuwasilisha nakala halisi ya hati ya malipo ya Benki [Bank Pay-in Slip, original copy] na kupata stakabadhi ya Halmashauri kwa zabuni iliyoombwa. Malipo yaliyotolewa kama ada ya maombi ya zabuni hayatarejeshwa.
7. Zabuni zote zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri [seal], na juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja **NAMBA YA ZABUNI** zipelekwe katika sanduku la zabuni lililoko katika ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji chumba namba 66 kwa kutumia Anuani ifuatayo:-

Katibu wa Bodi ya Zabuni

**Halmashauri ya Jiji,
Barabara ya Boma,
S.L.P. 3013, Arusha.**

8. Muda wa mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni **Tarehe 25.6.2018 siku ya Jumatatu saa 4:00 asubuhi**. Maombi yote yatafunguliwa muda mfupi baadaye na kwamba waombaji wote au wawakilishi wao wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo.
9. Halmashauri ya Jiji la Arusha hailazimiki kukubali/kutokukubali kutoa zabuni kwa mwombaji zabuni yeyote kutokana na kigezo cha malipo makubwa/malipo kidogo ya zabuni.

**MKURUGENZI
HALMASHAURI YA JIJI.**